Date Printed: 04/23/2009

JTS Box Number: IFES_73

Tab Number: 4

Document Title: Shiriki katika uchaguzi wa vionguzi

Document Date: 1994


Document Country: Tanzania

Document Language: Swahili

IFES ID: CE01889

*BD8A3E56-B52D-4B2E-8128-A08A204EA915*

# SHIRIKI KATIKA UCHAGUZI WA VIONGOZI



**TUMIA HAKI YAKO**

Kijitabu hiki kimeandaliwa ili kumwezesha mwananchi kuelewa wajibu na haki yake ya uraia katika suala zima la uchaguzi wa Wilaya na Miji, Bunge na Rais.

Suala la kujiandikisha kupiga kura na kufuatilia maelezo yatolewayo na Tume ya Uchaguzi katika hatua mbali mbali za uchaguzi ni muhimu katika kudumisha demokrasia ya kweli. Haki ya kuchagua viongozi ni kati ya haki muhimu za binadamu zinazotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa.

Mwananchi unapojiandikisha kupiga kura na ukajitokeza kupiga kura huwa umetoa mchango wako katika kuimarisha demokrasia.

Katika uchaguzi wa vyama vingi vya siasa kila mwananchi anayo haki ya kuchagua mgombea wa chama anachokipenda bila kushurutishwa au kurubuniwa. Hivyo ni haki ya mpiga kura kumchagua mgombea anayemuona kuwa ana uwezo bila kujali rangi, dini au kabila.

Kijitabu hiki kimeandaliwa kumsaidia mpigaji kura na hakina uhusiano wowote wala upendeleo wa chama cho chote cha siasa. Lengo ni kumwezesha mpiga kura kusoma na kufuatilia picha zilizomo ili kutambua uwajibikaji wake katika hatua mbali mbali za upigaji kura. Msomaji anashauriwa kutumia pamoja na wenzake elimu iliyomo kwenye kijitabu hiki.

**KWA NINI KUPIGA KURA NI HAKI YAKO?**

1. Baada ya kutimiza umri wa miaka 18 raia anao wajibu na haki katika taifa lake. Mojawapo ya wajibu ni kushiriki katika kuchagua viongozi na kuchaguliwa kuwa kiongozi.

2. Uchaguzi ndio unaotuwezesha kupata watu ambao watatuwakilisha Bungeni na katika Halmashauri za Wilaya na Miji.

3. Haki ya kupiga kura ni kati ya haki za msingi za binadamu zinazotambuliwa na Umoja wa Mataifa.

**ESAURP'S COUNCIL FOR DEMOCRACY**

**TEMA Publishers Company Limited**
S.L.P. 63115
DAR ES SALAAM

© The Eastern and Southern African Universities Research Programme (ESAURP) - Regional Council for Democracy, 1994

*Chapa ya Kwanza, 1994*

ISBN 9987 25 001 7

Haki zote zimehifadhiwa. Hairusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigisha chapa au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya TEMA Publishers Company Ltd.




Mwelekezaji anawahakikishia wakulima kuwa haki ya kupiga kura ni haki ya kila raia mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea.




**Akina mama ni vyema wakajitokeza kwa wingi kugombea uongozi ili kutumia haki yao ya kikatiba ya asilimia 25 na zaidi ya uwakilishi katika Halmashauri za Wilaya na Miji na asilimia 15 katika Bunge.**




**Usipojiandikisha kupiga kura hutaruhusiwa kupiga kura.**




**Sifa za uongozi ni mojawapo ya vigezo muhimu vya kumpima mgombea.**




**Mwelekezaji anatoa maelezo ya kushiriki katika uchaguzi kwa wafanyakazi wa kiwandani.**




**Mwelekezaji anawaelezea kwamba ni vyema kuchagua kiongozi bila kurubuniwa au kushurutishwa na mtu yeyote hasa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa.**




**Wanavyuo wanapata ufafanuzi juu ya uhusiano kati ya demokrasia ya vyama vingi na maendeleo.**




Kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi.




Watu hawa walifuatilia utaratibu wa kujiandikisha na kupiga kura ili kumpata kiongozi bora kwa maendeleo ya taifa.




**Kila mara jikumbushe mambo muhimu wakati wa kupiga kura.**




**Jiandikishe kupiga kura, toa majina yako kamili na jibu kwa ufasaha maswali yote unayoulizwa.**




**Hudhuria mikutano ya maelekezo ya uchaguzi kama inavyotolewa na Tume ya Uchaguzi.**




**Shiriki katika uteuzi wa mgombea ambaye utataka awe mwakilishi wako.**




**Ni muhimu kuhudhuria mikutano ya kampeni za uchaguzi.**




**Kuwa msikivu na mtulivu kwenye mikutano ya kampeni, wasikilize wagombea ili uweze kuwapima uwezo wao.**




**Epuka kushiriki katika vitendo au mazungumzo ya uhuni na matusi dhidi ya wagombea au wale usiokubaliana na mawazo yao.**




**Kupiga kura kuna kupa wewe mwenyewe fursa ya kuamua ni akina nani wawe viongozi.**




**Hakikisha unawahi kupiga kura katika muda uliopangwa.**




Piga kura kwa siri.




**Tumbukiza kwenye kisanduku kinachohusika**




**Pokea matokeo ya uchaguzi na uyakubali.**




Uchaguzi wa viongozi bora unaimarisha huduma za watoto, akina mama na taifa kwa jumla kwa kuboresha huduma za jamii kama Afya, Elimu n.k.

TEMA

TEMA PUBLISHERS CO. LTD.
DAR ES SALAAM

ISBN 9987 25 001 7